

Kuwafuatilia Wagonjwa wa COVID-19: Utaratibu

Huenda umesikia kuwa kuwafuatilia wagonjwa ni njia moja ya kuzuia kusambaa kwa ugonjwa wa COVID-19.

Lakini kuwafuatilia wagonjwa ni nini?

Kuwafuatilia wagonjwa ni kuwatafuta watu ambao wanaweza kuambukiza ugonjwa wa COVID-19 – na hawajui – na kuwashauri wakae nyumbani na mbali na watu wengine ili wasimwambukize mtu yeyote mwingine.

Baada ya mtu kuwa kwenye hatari ya kuambukizwa ugonjwa wa COVID-19, anaweza kuanza kuusambaza kwa watu wengine kuanzia siku 2 hadi 14 baadaye. Katika kipindi hiki, huenda mtu asijsikie mgonjwa lakini bado anaweza kuwaambukiza watu wengine ugonjwa wa COVID-19.

Hivi ndivyo watu wengi zaidi wanavyoambukizwa.

Ufuatiliaji wa wagonjwa ni njia moja ya kukomesha mchakato huu.

Utaratibu wake ndio huu:

Idara ya Afya ya Minnesota inaarifiwa kuhusu kila mtu anayetambuliwa kuwa na virusi vya COVID-19, kama inavyofanyika kwa ugonjwa wa ukambi pia. Ukitambuliwa kuwa na ugonjwa wa COVID-19, unaweza kutarajia kupigiwa simu kutoka kwa mtafiti wa mtu aliye na COVID-19. Wakati mwingine mtu huyu pia huitwa mfuatiliaji wa wagonjwa. Watafiti huifanyia kazi idara za afya ya umma za jimbo, serikali ya mitaa au ya kabila.

Watafiti hupiga simu kukupa maelezo kuhusu COVID-19, kukuuliza kuhusu afya yako, na kujibu maswali yako. Kwanza watakusomea maelezo yanayoitwa Onyo la Tennessee. Haya ni maelezo kuhusu faragha na yanakuuliza kama unakubali kushiriki maelezo yako ya kiafya. Maelezo yako hayawezi kushirikiwa kwa mtu yeyote bila idhini yako.

Pia watakuuliza ulikaribiana na nani siku chache kabla ya kutambuliwa kuwa na virusi hivi. Kwa ujumla, mtu yeyote ambaye amekaa kwa zaidi ya dakika 15 akiwa amekaribiana na mtu aliye na COVID-19 huwa katika hatari ya kuambukizwa. Mtafiti wa wagonjwa atakusaidia kujua ni nani anayechukuliwa kuwa mtu aliye katika hatari ya kuambukizwa.

Watafiti wa wagonjwa wanaweza kuwapigia simu watu uliokaribiana nao na kuzungumza nao kuhusu kupimwa. Hawatahiriki jina lako au maelezo mengine yoyote ya kibinafsi na watu uliokaribiana nao bila idhini yako. Watawambia wakae nyumbani kwa siku 14, wakihesabu kutoka mtu wa mwisho aliyekaribiana na wewe. Wakikaa nyumbani, viini vyao pia vitabaki nyumbani.

Kufuatilia wagonjwa kutafanikiwa tu kwa usaidizi wako.

Mtafiti wa wagonjwa akikupigia simu, hakikisha umeichukua. Ukikosa kuchukua simu yao, watakutumia ujumbe. Hakikisha umewapigia baadaye.

Watafiti wa wagonjwa watakuafahamisha wao ni kina nani, wanafanya kazi wapi, na kwamba wanapigia simu kuhusu COVID-19. Hawatawahi kukuuliza kuhusu hali yako ya uhamiaji, hawatakuomba pesa, wala nambari za akaunti yako ya benki, kadi ya mikopo, nambari za usalama wa jamii

KUWAFUATILIA WAGONJWA WA COVID-19: MAANDISHI YA UTARATIBU

Ikiwa hutaki kuzungumza kwa Kiingereza, mfahamishe mtafiti wa wagonjwa anayewasiliana nawe. Watamtafuta mhojiwa tofauti anayezungumza lugha yako au wakutumie mkalimani wa njia ya simu.

Watafiti wa wagonjwa pia watakupa maelezo – kama vile jinsi ya kuwalinda watu unaokaa nao na jinsi ya kutafuta chakula, dawa, na vitu vingine unavyohitaji kukaa salama nyumbani.

Pamoja, tukisaidiwa na watafiti wa wagonjwa na kufanya ufuatiliaji wa wagonjwa, tunaweza kupunguza kusambaa kwa ugonjwa wa COVID-19. Asante kwa kutimiza wajibu wako.

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

19/10/2020 (Swahili)

Ili upate maelezo haya kwa muundo tofauti, piga simu: 651-201-4989